**Mchezo Wa Subira**
**Sadia Ashraf (Edited by Logan Cochrane, Translated by Eric Nyaga)**

**Noah na Orene si mabikira, lakini hawajawahi kufanya mapenzi mmoja na mwingine.**
**Noah anahisi tayari kufanya Mapenzi na Orene, lakini Orene anataka kusubiri.**

**Noah**: Orene sote wawili tumewahi kufanya mapenzi hapo mbeleni, ni nini kinacho tuzuia kufanya mapenzi mimi na wewe?

**Orene**: Hakuna kinacho tuzuia. Tumechagua kusubiri. Muamuzi ndilo jambo la maana.

**Noah**: Je, hutaki Kufanya mapenzi na mimi?

**Orene**: Ndio nataka ... ninatamani. Lakini nataka kusubiri hadi niwe tayari.

**Noah**: kuhisi tayari juu ya nini? Wewe si bikira.

**Orene**: Haijalishi. Nimechagua kusubiri. Nimesema hili wazi kwako hapo mbeleni. Ngono ni mpango mkubwa. Mimi nataka kusubiri. Unahitaji kuelewa labda sitakuwa tayari hadi wakati wa ndoa.

**Noah**: Lakini si ngono ni njia bora zaidi ya kuonyesha jinsi tunavyo jali mmoja mmoja na mwingine.

**Orene**: (anaonekana kuwa na wasiwasi) nani aliyekuambia hayo?

**Noah**: (anainua mabega) Baadhi ya marafiki zangu.

**Orene**: (anatikiza kichwa chake) Naam wamekosea.

**Noah**: Lakini walisema ...

**Orene**: Vile unavyo heshimu matakwa yangu na kusubiri hadi niwe tayari inaonyesha vile unavyonijali. Kuna njia nying za kuonyesha nguvu za hisia zetu. Ngono si bora au njia pekee ya kuonyesha kina cha hisia zetu.

**Noah**: Siyo?

**Orene**: (Anacheka) Hapana! Unajua kiasi ninavyo kujali, sivyo?

**Noah**: (anatabasamu) Ndio. Umeonyesha wazi mara moja au mbili.

**Orene**: (anamdukiza) Na hatujafanya mapenzi, ndivyo ...?

**Noah**: Hapana

**Orene**: (akitabasamu) hasa.

**Noah**: Kwa hivyo tusubiri?

**Orene**: (akishika mkono wake) ndio tusubiri.

**Kuzungumza kuhusu ngono ni njia bora ya kujua hisia za mtu mwingine kuhusu ngono na kubadilishana mawazo yako mwenyewe. kama Orene una haki ya kufanya hisia zako wazi. Kuzungumza na mtu mnaye fahamiana - kama rafiki wa karibu - kuhusu ngono inaweza kukusaidia kuelezea wasiwasi au hofu au hata shinikizo unazo hisi kufanya mapenzi. Ikiwa umekuwa ukifanya mapenzi kabla ya hii haina maana lazima utajisikia vizuri kufanya mapenzi tena, hata na mtu yule mmoja. Kamwe usihisi shinikizo la kufanya chochote pasipo kwa hiari.**

**Wazo la Maarifa**
**Sadia Ashraf**

**Baada ya kumuona Noah, Orene anatembea kuelekea nyumbani na anakutana na Benjamin - rafiki wa Noah. Yeye ana wivu kwamba Orene ana uhusiano na Noah. Benjamin kwa kutofahamu anaamini kwamba kufanya mapenzi na wasichana wengi ni jambo hodari kufanya.**

**Benjamin**: Ngojea, Orene!

**Orene**: (anageuka) Oh hujambo, Benjamin. Sikuwa nimekuona.

**Benjamin**: (anakimbia ndio amfikie) Vyema kukuona hapa.

**Orene**: Ndio. Ninarejea kutoka nyumbani kwa Noah.

**Benjamin**: (anaunganisha mkono wake na ule wa Orene) Oh ni sawa. Mimi kamwe sielewi kwa nini unampenda Noah.

**Orene**: (Anacheka) Kwa nini?

**Benjamin**: Kuna wavulana bora kuliko Noah.

**Orene anaanza kujisikia mwenye wasiwasi kushirikiana na Benjamin. Yeye hana imani naye.**

**Orene**: (akijaribu kujiondoa kutoka kwa mkono wa Benjamin) Sielewi unavyo maanisha.

**Benjamin**: Wavulana kama mimi.

**Orene**: (Anacheka).

**Benjamin**: (Anacheka) Ni utani tu. Tabasamu!

**Orene**: Mcheshi sana. Inanilazimu kuelekea nyumbani sasa.

**Benjamin**: Kwa nini haraka hivyo?

**Orene**: (anaondosha mkono wa Benjamin kutoka kwa wake) nina kutana na ndugu yangu na sitaki kuchelewa.

**Benjamin**: (anapiga teke jiwe lililo sakafuni) Je, mimi si mzuri vya kutosha kwa ajili yako?

**Orene**: Benjamin ni nini kilichokuingilia? Sitaki kuchelewa ni hayo tu.

**Benjamin**: (Anajaribu kuchukua mkono wa Orene) Kawia kidogo na mimi. (anasimama na huanza kumuelekeza Orene kwenye kona)
**Orene**: (anapatwa na hofu) Benjamin unafanya nini?

**Benjamin**: Ninakuonyesha jinsi ninavyo kupenda. Zaidi ya Noah.

**Orene anatambua kwamba yuko katika hali ya hatari. Anajua kuwa anahitaji kumpurukusha Benjamin.**

**Orene**: (Akitabasamu) tayari najua unavyo nipenda. Ndiposa sisi ni marafiki.

**Benjamin**: (Akitabasamu pia) Naam.

**Orene**: (Akionyesha na akipunga juu ya bega la Benjamin) Oh Thomas. Thomas! Hujambo Thomas! Benjamin, ndugu yangu ...

**Benjamin**: (Anageuka)

**Orene anatoroka. Ndugu yake hakuwa hapo kamwe. Anakimbia mpaka kwa sehemu ya mji penye watu wengi ambapo atakuwa salama.**

**Licha ya kufanya hisia zako wazi, wakati mwingine watu hawataki kukusikiliza. Kama mtu hasikilizi kwamba una haki ya kusema la kwa ngono, ni haki yako ya kusimama imara na hisia zako. Kufikiria kwa haraka kama Orene ni muhimu katika kumpurukusha mtu anaye jaribu kukulazimisha kufanya kitu ambacho hutaki kufanya, kwa mfano kufanya mapenzi.**

**Tayari, Jipange, Nenda**
**Sadia Ashraf (Edited by Logan Cochrane, Translated by Eric Nyaga)**

**Wakati umepita, na Orene na Noah ni wachumba na wataoana hivi karibuni. Orene huko tayari kufanya mapenzi sasa na anatazamia kwa hamu usiku wa harusi. Noah alisubiri kwa uvumilivu na ana furaha hakukosa kumuhesima Orene na kujaribu kumulazimisha. Anadhani mapenzi yatakuwa maalum zaidi sasa wawili hao wakiwa tayari.**

**Orene**: Noah...

**Noah**: Naam?

**Orene**: Nadhani niko tayari kufanya mapenzi na wewe.

**Noah**: (Anacheka) Naam, ni vizuri kuona kwamba sisi tutafunga ndoa hivi karibuni.

**Orene**: (Anatabasamu) Ndio. Tume thibitisha kwamba tuna nia ya dhati kati yetu. Mimi niko tayari.

**Noah**: Nina furaha kwamba uliniambia haukuwa tayari hapo mbeleni. Ni muhimu kushiriki hisia zetu.

**Orene**: Ndio, asante kwa kufahamu. Usiku wa harusi yetu utakuwa wa ajabu.

**Noah**: (Akichukua mkono wake) Ndio.

**Orene**: Una hofu?

**Noah**: kidogo.

**Orene**: Mimi pia. Lakini nina furaha tunaweza kujadili jinsi tunavyohisi, tusingefanya hivyo ningekuwa na hofu zaidi.

**Noah**: (Akitabasamu) Ninajua. Ngono ni hatua kubwa. Kama hatuko tayari kujadiliana juu yake basi nadhani hatuko tayari kufanya mapenzi.

**Orene**: (Akitabasamu) Umesema ukweli.

**Noah**: Mimi daima husema ukweli!

**Orene**: (Anacheka) Hapana! Sio wakati uliniuliza kama ngono ilikuwa njia bora zaidi ya kuonyesha tunavyojali mmoja kwa mwingine.

**Noah**: sawa, sawa. Mimi sisemi ukweli kila wakati ...

**Orene**: Basi, kwa sababu tuna nia ya dhati kati yetu hatuna haja ya kutumia kondomu, sivyo?

**Noah**: (akionyesha kustuka) Orene, tunapaswa daima kutumia kondomu wakati tunafanya mapenzi.

**Orene**: Kwa nini?

**Noah**: Ili kujilinda kutokana na magonjwa kama vile VVU / UKIMWI. Kondomu zitatusaidia kukaa kwa afya na usalama.

**Orene**: Lakini ... watoto ... wewe ulisema ... ulisema unataka watoto. Sisi ... tulikubaliana ... tulikubaliana kwamba tunataka watoto.

**Noah**: Mimi sijabadili mawazo yangu Orene, bado nataka watoto. Ndio maana tunahitaji kufanya ahadi kwamba tutaweza kupata kupimwa mara kwa mara pia.

**Orene**: Kupimwa? Noah nini kinaendelea?

**Noah**: Ngono si njia pekee ambayo tunaweza kupata VVU. Tunaweza kupata kutoka kwa damu ya mtu mwenye VVU, kama damu yao ikichanganywa na yetu - tukijikata wenyewe au kwa njia ya sindano. Ajali hutokea. Nakupenda Orene - sitaki kupata wagonjwa. Niahidi kwamba tutaweza kupima mara kwa mara ili kuhakikisha tuko wenye afya.

**Orene**: Nina kupenda pie, lakini hatuna VVU ... sisi ni wenye afya. Sisi ni waaminifu...

**Noah**: Ndio, sisi ni waaminifu. Na ndio, sisi ni wenye afya. Je, hutaki kuhakikisha tumesalia hivi? Pamoja na kupimwa mara kwa mara tutahakikisha bado tuko wenye afya. Niahidi ... tafadhali ...

**Orene**: Sawa ... nakuamini Noah. Nita pata ... mimi ninakuahdi tutaweza kupata kupimwa.

**Noah**: sio tu kwa ajili ya afya zetu. Ni kwa ajili ya maisha yetu ya usoni. Kama mama ana virusi vya ukimwi anaweza kuvipitisha kwa watoto wake. Hatutaki kuhatarisha hayo, ndivyo?

**Orene**: Hapana! Mimi nataka kupata watoto wengi wenye afya nzuri na wewe. Mimi na ahidi Noah. Na ahidi kwenda kupimwa.

**Noah anasema ukweli, Ngono sio njia ya pekee unayoweza kupata VVU. Lakini, kama wewe na mpenzi wako na mumejadiliana kuhusu ngono, na kuamua kufanya mapenzi, basi lazima kuhakikisha daima mumetumia kondomu ili kujikinga wewe na mpenzi wako kutokana na magonjwa kama vile VVU / UKIMWI. Pia ni muhimu kupimwa mara kwa mara kwa ajili ya VVU ili kuhakikisha wewe na mpenzi wako mko salama na mwenye afya.**

**Noah na Orene walitumia *Tayari, Jipange, Nenda* kama sheria yao:**

***Tayari***
**Kamwe usikimbilie kufanya mapenzi. Kusubiri kufanya ngono si jambo mbaya - kwa kweli ni njia bora zaidi ya kukulinda kutokana na VVU / UKIMWI. Hakikisha kwamba una hiari na wazo la kufanya mapenzi; zungumza kuhusu hilo, na wala usihisi kushinikizwa - hakikisha ndivyo unavyotaka kufanya.**

***Jipange***
**Kama umeamua kufanya mapenzi, hakikisha unatumia kondomu kujiweka wewe na mpenzi wako salama. Ngono bila kondomu inaweka afya yako na ya mpenzi wako katika hatari kubwa. Pia, kupimwa mara kwa mara kwa ajili ya VVU ni hatua muhimu katika kuishi kwa afya na usalama.**

***Na hatimaye, Nenda***
**Kama wewe umeamua kufanya mapenzi, unapaswa kuendelea tu kama nyote wawili munajisikia tayari na mumejipanga.**